- Yesu ajaze moyo upendo wake Mtakatifu. Jipe moyo. Fanya kazi kwa ajili ya Yes una Maria na utazamie daima kutoa uhai wetu kwa ajili ya roho zinazogharimu Damu ya Yesu, shughulika ili uwe mtakatifu. (Kitabu cha barua no. 3 – 832)
- Mungu akujaze upendo wake na akutakatifuze ndani yake nakubariki. (Kitab cha Barua no. 3 – 904)
- Kumbuka kwamba Mungu amekuita katika Shirika hili Takatifu ili uwe Mtakatifu, na kutakatifuza roho za wengine ambazo zinagharimu Damu ya Kristo Msulibiwa Mchumba wetu Mtakatifu… (Kitab cha Barua no. 3 – 909)

Tafakari ukimya

Kushirikishana

Wimbo: Ubi caritas

**Tusali siku kwa shukrani ya Wito kwa Utakatifu:Preghiamo nel giorno del Ringraziamento per la nostra Vocazione a favore della santità:**

Mungu wa upendo na huruma, tunakushukuru kwa kutuita kuishi maisha ya wakfu kwa ubatizo kwa kujitoa maisha yetu yote kwako ili kukuabudu na kwa upendo kuhudumia kwa wengine.

Utusaidie tufungue mioyo yetu kwa Roho Mtakakatifu ili tuweze kujazwa upendo kamili. Tunaomba neema tunayohitaji kupekea kutoka kwako ule utakatifu ambao ulituitia katika Shirika hili. Kwamba maisha yetu yawe sura hai na ushuhuda wa upendo mororo kwa ajili ya binadamu wote, ili tuweze siku nzima katika kukuabudu na katika kuhudumia kwa furaha, tukisaidia uumbaji wote katika mwendo kuelekea kwenye ule mpango mzuri wa vitu ambao Mwanao Yesu amekuja kuuthibisha kwa Damu yake.

Ututakatifuze Roho Mtakatifu wa Mungu, na kutumba daima tufanane zaidi na Kristo wa pasaka. Amina.

**Wimbo wa Maria:** (wowote)

**SALA YA PAMOJA KWA MAADHIMISHO YA KUTANGAZWA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS**

**"Wajitakatifuze wote, hivi siku moja Yesu mwema atatuunganisha katika utukufu wake, uniamini".** (Kitabu cha Barua no. 3 - 301)



**Utangulizi:**

Maria ameongea mara nyingi juu ya wito wetu wa kuwa watakatifu. Wakati tunaadhimisha utakatifu ambao Mungu alimwongoza Maria, tutafakari kuhusu wito wetu wote kuelekea utakatatifu na juu ya maana yake kwetu na kwa ajili ya ulimwengu tulipo.

**Utenzi:** Wimbo wa Sifa kwa Damu ya Kristo. Enyi watu wote…

**Kutoka Mwanga wa Mataifa:** (nn. 40-41)

**Wito wa Kanisa zima kwenye utakatifu**

Bwana Yesu, Mwalimu na mfano wa Mungu wa kila utimilifu, kwa wote na kila mmoja wa mitume wake wa kila hali alihubiri ule utakatifu wa maisha, ambao yeye mwenyewe ni muumba na mkamilishaji: ″Basi muwe wakamilifu kama alivyo mkamilifu Baba yenu wa Mbinguni" Kweli kwa wote alimtuma Roho Mtakatifu, aliyewaongoza kutoka ndani kumpenda Mungu kwa moyo wote, kwa roho yao yote, kwa akili yao yote, kwa nguvu zao zote na kupendana kati yao kama Kristo alivyowapenda. Wafuasi wa Kristo, walioitwa na Mungu sio kwa heshima ya kazi zao, bali kwa heshima ya kusudi lake na kwa neema yake, wakifanywa wenye haki katika Kristo Yesu Bwana wetu, katika ubatizo wa imani walifanywa kweli wana wa Mungu na washiriki wa asili ya Mungu, na kwa hiyo ni watakatifu halisi. Kwa hiyo wao, kwa msaada wa Mungu, wabaki na kukamilisha kwa maisha yao utakatifu walioupokea. Aliwaonya Mitume waishi ″Kama wanavyopaswa kuishi watakatifu" wajivike "Kama iwapasavyo wateule wa Mungu, wakatakatifu na wapendwao, moyo wa huruma, wema, unyofu utulivu na uvumilivu″ na wazae matunda ya Roho kwa ajili ya kujitakatifuza.

Wimbo: Ubi caritas

Ni wazi kwa kila mtu, kwamba wote wanaoamini katika Kristo katika hali yoyote au lolote, wameitwa kwenye ukamilifu wa maisha ya Kikristo na kwenye utimilifu wa upendo na kwamba utakatifu ule unaendelea katika jamii yenyewe ya dunia ni mwendo wa maisha ya kiutu zaidi. Ili tufike kwenye utimifu huu waamini wanatumia nguvu walizopokea kulingana na kipimo ambacho Kristo anataka kuwatunukia, ili kwa wakifuata mfano wake na kufananishwa na sura yake katika yote, wakitii mapenzi ya Mungu Baba, kwa ukarimu wote, wanajiweka wakfu kwa utukufu wa Mugu na kwenye kumhudumia jirani. Huu ni utakatifu wa watu wa Mungu utakua na kuzaa matunda ya kutosha, kama inavyoonesha kung`arishwa historia ya Kanisa kutokana na maisha ya watakatifu wengi.

Wimbo: Ubi caritas

Vyanzo mbalimbali vya maisha na shughuli mbalimbali katika mwuungano na watakatifu umetunzwa na wale ambao wameguswa na Roho wa Mungu na watii kwenye sauti ya Mungu Baba na wakiabudu katika roho na kweli ya Mungu Baba, wanatembea nyuma ya Kristo maskini, myenyekevu na mwenye kubeba Msalaba, ili kustahili kushiriki pamoja naye utukufu wake; Kila mmoja kulingana na vipaji yake na kazi rasmi inayopaswa kusonga mbele bila kurudi nyuma kwa njia ya imani hai, inayowashwa tumaini na kufanya kazi kwa njia ya upendo.

Wimbo: Ubi caritas

Ukimya tafakari

**Maria anatuambia nini?**

Maria anatualika kutafakari juu ya tunu ya wito wetu kama Waabuduo Damu ya Kristo na jinsi tunavyoishi, sio kwa ajili yetu tu, bali kwa ajili ya watu wote wa Mungu. Tusikilize Maneno yake na tujiweke wazi kwenye Neno linalogusa zaidi moyo wetu…

- Tumtumikie Mungu kwa upendo, na tujitakatifuze, binti, huu ni wito wetu. Yesu na Maria daima wawe daima mioyoni mwetu. (Kitab cha Barua no. 1 - 229
- Tupo pamoja binti yangu, katika kumpenda Yesu kwa moyo na katika kutunza kwa ajili ya roho za jirani yetu. (Kitab cha Barua no. I - 244)
- ...Tujitakatifuze na tusichoke kuwatakatifuza wengine. (Kitab cha Barua no.l 2 - 397)
- Uwe na furaha mwanangu; Yesu anatupenda, na Mama yake, ni Mama yetu mpendwa anatutaka tuwe watakatifu, hatakosa kutupatia misaada ya lazima: na tutakuwa watakatifu? Ndiyo, hata sisi tukitaka; kwa sababu hii tumekuwa Waabuduo wa Damu Takatifu kwa sababu tunataka. Basi jipe moyo na kudumu (Kitab cha barua no.2 - 582)
- Tumtumikia Mungu Mbarikiwa, na tujitahidi kumfahamisha Yesu Msulibiwa kwa upendo wetu wote ili wengi wampende, sio kuwasikitisha… tuwe watakatifu kwa kumpenda sana Yesu mpenzi wetu. (Kitab cha Barua no. 2 - 617)
- Upendo wa Yesu ujae moyoni mwako na uwe mtakatifu haraka. (Kitab cha barua no. 3 - 740)